



RIPOTI YA MWAKA MUHTASARI RASMI WA
KAMATI YA UENDESHAJI NA YA
MKURUGENZI WA KITUO CHA MAELEZO
YA AFYA YA JAMII ZA TABAKA ZA WALIO
WACHACHE

2002 – 2003

MUHTASARI RASMI

Makaratasi haya yana maelezo kuhusu Ripoti ya Mwaka ya Kamati ya Uendeshaji cha Kituo cha Maliasili ya Taifa kwa ajili ya Afya ya Tabaka za Walio Wachache na Ripoti ya Mkurugenzi wa NRCEMH na kikundi chake. Kikundi Kisimamizi kinatoa maarifa na mwelekeo yatakayotumiwa na NRCEMH, kina wanachama wenye ujuzi waliopo nchini Scotland. Ripoti hii ya pamoja inaonyesha uhusiano wa kikazi kati ya Kikundi Kisimamizi na NRCEMH ambao umetimizwa.

Ripoti hii imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaeleza shughuli za NRCEMH. Sehemu ya pili inaelezea kuhusu maendeleo yaliyofanywa na NHSScotland ili kutimiza sera za tabaka na afya, haswa zile zinazofuatana na matakwa ya Barua ya Idara ya Afya ya kuhusu Haki bila Upendeleo (HDL) (2002) 51. Ripoti ya Maendeleo ya Haki bila Upendeleo, katika sehemu ya pili inaelezea mojawapo ya sera za NRCEMH baada ya kuanzisha FFA mradi wa mwaka 2000. Kiliangalia namna na jinsi ya kufuatilia ukuzaji wa haki bila upendeleo katika mwaka wa kwanza kulingana na shughuli fulani za Uhusiano kati ya Jamii tofauti (Marekebisho) Kifungu 2000 (RRAA). Pamoja na utaratibu huo kulikuwa na ukaguzi uliofanywa na FFA Action Plans kufuatana na HDL (2002) 51.

Pamoja na uchunguzi wa utendaji, pia kinajadili matokeo muhimu na mapendekezo yatakayosaidia Kamati ili zianze kutekeleza mipango yao na kufanya makadirio ya maendeleo kwenye eneo fulani.

Utaratibu wa Uchambuzi Nchini ulitayarishwa ili kufanya uchunguzi na tunategemea unaweza kuwa muongozo bora kwa Kamati na Tume. Katika mwaka wa kwanza wa NRCEMH pamoja na CRE zilisaidiwa na ziliweza kufuatilia masharti mapya, kubadilishana mawazo na kuhimiza njia bora za utendaji wa kazi katika Mitandao ya Taifa. Lengo kubwa la mwaka ujao utakuwa ni kuachana na sera za maendeleo na kuzingatia sera za utekelezaji.

Kitangulizi

Shughuli hii inafuatilia masharti ya RRAA 2000 pamoja na Haki bila Upendeleo HDL. Kinafuatilia kwa dhati majukumu ya ujumla ya NHSScotland yanayohusu mipango ya jumua, haki bila upendeleo na usambazaji pamoja na Kuzingatia Wagonjwa na Ushirikiano wa Umma (PFPI).

SEHEMU YA 1

Kituo cha Maelezo ya Afya ya Jamii za Tabaka za Walio Wachache {The National Resource Centre for Ethnic Minority Health (NRCEMH)} kiliundwa na Kamati ya Scotland ili isaidie NHSScotland, lakini nia yake haswa ni kusaidia Kamati za Afya ili kutoa utaratibu wa afya kwa jamii za tabaka za walio wachache. NRCEMH ilianza kazi zake mnamo tarehe 1 April 2002. Kina Mkurugenzi, Makatibu wawili wa Mradi na Wakurugenzi watatu wa Mradi wanaozingatia masuala muhimu ya sera, maelezo na mafunzo. Pamoja na hayo, NRCEMH imetambua mapema umuhimu wa kuongezea suala lingine la kuzingatia la maendeleo ya jumua.

Msimamo wa NRCEMH ni kusaidia ili kuhakikisha kuna utoaji wa huduma bora na kutilia maanani mashaka ya jamii za tabaka za walio wachache na kusaidia maendeleo ya huduma zinazohitaji kufuatilia kwa dhati mila na desturi zinazoambatana na sera na utendaji wa kuleta haki bila upendeleo.

Utekelezaji wa sera

Mwaka uliopita NRCEMH ilisaidia kukuza Kamati na Tume zote zilizopo nchini Scotland ili ziendeleze Taratibu za Haki bila Upendeleo wa Rangi (Race Equality Schemes) na Mipango ya Haki bila Upendeleo pamoja na kusimamia utaratibu wa Maangalizi Mapya Nchini ikishirikiana na CRE.

NRCEMH ilifanya utendaji mzuri wa kuendeleza ushirikiano wa kikazi na CRE, ambayo imetoa taarifa ya pamoja ya kuunga mkono mashirika ya afya yaliyopo katika maeneo mengine matatu ya Uingereza. Utaratibu huu uliotimiza mfumo wa kuvutia unaotumika nchini Scotland unaweza kuonyesha jinsi masuala ya afya yanavyoweza kuongoza katika masuala ya haki bila upendeleo na kufuta ubaguzi. Matokeo ya ushirikiano huo ni utendaji bora wa kazi unaoambatana na uongozi bora pamoja na moyo wa kutenda kazi unaonyeshwa na wakubwa. Utaratibu huu utapunguza vizuizi na kuangalia sera zote na mipango yote inayohusiana na jamii mbali mbali.

Uchunguzi uliofanywa katika ripoti inathibitisha ya kwamba kuna maendeleo tangu mkutano wa Fair For All Stocktake ufanywe miaka miwili iliyopita. Kamati na Tume kadhaa zimeteteleza kwa bidii na kwa moyo na kufuatilia masharti waliopewa, ingawa inasikitisha kujua kwamba wengine wanakamilisha kazi zao bila kuwa na moyo au bidii ya utendaji. Utoaji wa Taratibu za Haki bila Upendeleo (Race Equality Schemes) na Mipango ya Utekelezaji ni dhahiri kwamba zimesaidia vyama vyingi na watu kadhaa waweze kuelewa chanzo cha ubaguzi serikalini ili waweze kukuza usimamizi bora na mabadiliko yanayoendana na mila na desturi. Kwa wengi, hili ni jambo jipya, uwezo wao na imani yao utakuzwa baada ya muda. Bado kuna changamoto ya kufikisha juhudi hizo kwa wafanyakazi wote na wajumbe wote wa kamati, pamoja na kujenga uaminifu na imani katika jumua, ili kuweza kutekeleza mpango wa afya katika jamii za tabaka za walio wachache.

Pamoja na majukumu ya kisheria na ya utendaji wa Kamati, masuala kadhaa muhimu yamechaguliwa ili yaangaliwe. Masuala haya yalizingatiwa, haswa yale yanayohusiana na umuhimu wa kushirikiana na wa kuchochea utaratibu mzuri wa kutenda kazi. Hivyo, tungependa kushirikiana na Wazururaji (Gypsy), Waombaji Hifadhi ya Kisiasa na Wakimbizi, Ustawi wa Jamii, Mashirika ya Afya ya Akili na Kansa:

Maendeleo ya Jumua: Kamati ya Uendeshaji kilitoa muongozo fasaha tangu awali na kwamba hatuo ya nne ya shughuli ya NRCEMH itakuwa ustawi wa jamii. NRCEMH iliunda kikundi cha utendaji kitakachoshirikiana na vyama vilivyopo vya jamii za tabaka za walio wachache ili waendeleze Utaratibu wa Kuzingatia Mgonjwa na Kushirikisha Jumua wakishirikiana na Utaratibu wa Kuzingatia Mgonjwa wa SEHD pamoja na Kitengo cha Kupima Ubora.

Afya ya Akili na Maisha bora/Madawa ya kulevya: Kamati ya Scotland imetambua matatizo ya afya ya akili kama ni suala muhimu la kuzingatia, kwa hiyo Kamati ya Ustawi ya Afya ya Akili itaangalia suala hilo itapofanya shughuli za mwaka huu. Ili kuweza kusaidia suala hili, inatarajiwa ya kwamba kutakuwa na mtandao nchini ambao utasaidiwa na awamu ya pili ya NRCEMH. Shughuli hii itaangalia maarifa ya hivi sasa yanayofanywa na Kamati pamoja na Tume na pia itaangalia jinsi mashirika hayo yanavyotenda kazi zao pamoja na kuangalia shughuli zao. Pia, uzingatiaji wa shughuli zinazofundisha ustawi mzuri wa afya ya akili kufuatana na mila na utamaduni wakati wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa idara ya afya na wa ustawi wa jamii zinaendelezwa.

Kansa: Kufuatana na ombi la CRE, NRCEMH ilikubali kutoa msaada wake wa kutoa ushauri unaohusiana na taratibu ya kupambana na kansa. Kikundi kilichoundwa na mashirika mengi kimeundwa ili kiendeshe shughuli zinazojishughulisha na ustawi wa jamii pamoja na umuhimu wa kukuza afya bora, ushirikiano kati ya vyama vya jamii za tabaka za walio wachache na njia bora ya kusimamia kila hatua. Mazungumzo ya mwanzo na Macmillan Cancer Relief yameshaanza ili tuweze kuchukua hatua ya pamoja na kuendeleza suala hili, pamoja na kutambua njia zinazofaa za kutatua masuala na matatizo yaliyopo.

Gypsy/Travellers: Mkutano wa Haki bila Upendeleo Stocktake uliofanywa 2000 ulionyesha idadi kubwa ya upungufu wa huduma, na wasiwasi kuhusu udhaifu wa msimamo wa kushirikiana na Wazururaji (Gypsy), Waombaji Hifadhi ya Kisiasa na Wakimbizi. Kuhusu Wazururaji (Gypsy), kulikuwa na mkutano uitwao National Roundtable mwezi Januari 2003, mkutano huo uliwapa nafasi wakilishi wa jumua kuanza kuzungumzia masuala muhimu ya afya. Maeneo yaliyozingatia ni pamoja na

uchapishaji wa makaratasi ya maelezo ya afya, uchambuzi wa mahitaji ya jumua na uambatanishaji wa kumbukumbu za afya kwa urahisi.

Waombaji Hifadhi ya Kisiasa na Wakimbizi: NRCEMH ilishirikiana na baraza la Kamati ya Scotland liitwalo Scottish Refugee Integration Forum (SRIF) ili kutayarisha Mpango ambao utafanikisha ujumuikaji wa Waombaji Hifadhi ya Kisiasa na Wakimbizi nchini Scotland. NRCEMH itakuwa na wajibu wa kuisaidia NHS kutekeleza masuala yalioandikwa kwenye ripoti ya SRIF ikiwa kama ni utaratibu wa kawaida wa FFA.

Mafunzo na shughuli za maendeleo

Lengo muhimu la utaratibu wa mafunzo ya NRCEMH ni kukuza njia za kuendeleza maarifa, mitazamo inayohusiana na mila na desturi pamoja na ujuzi wa wafanyakazi wa NHS ili waweze kutoa huduma nzuri zinazohusiana na mila na desturi. Utaratibu wa mafunzo na maendeleo unaendeleza ajenda ya maendeleo ya mafunzo kufuatana na mtizamo inayoambatishwa. Ratiba ya utekelezaji imetungwa na kugawanywa kwa vikundi vitatu vifuatavyo: ujuzi na maarifa; kuthamini tofauti na mitazamo inayohusiana na mila na desturi; pamoja na mawasiliano yanayofaa na matumizi/mkusanyiko wa maelezo ya jamii tofauti. Mafunzo yanayofanyika nchini yanahitaji kufanyiwa uchambuzi na wafanyakazi wa NHS wanaoishi Scotland wakishirikiana na Kamati ya Scotland kutayarisha taratibu za PFPI na FFA. Kielelezo kinachosaidia Kamati za Afya vinavyokuza mikakati ya mafunzo kinatayarishwa. Shughuli zilizopo ni pamoja na utoaji wa taarifa rasmi ya maendeleo ya mafunzo na kuendeleza uhusiano mzuri wa mila na desturi ukishirikiana na NHS Elimu Scotland.

Maelezo, uchambuzi na shughuli za utafiti

Kuna uhaba wa maelezo kamili wa jamii mbali mbali na masuala ya afya nchini Scotland na matokeo yake ni kwamba maamuzi ya sera na masuala muhimu yanafanywa kwa kutumia twakimu zilizopo nchini Uingereza na Wales. Lengo muhimu la NRCEMH ni kueleza kwa usahihi maelezo, utendaji wa kazi na kuorodhesha maelezo yanayohitajiwa na National Ethnic Health Data. Shughuli hii inajaribu kupambana na ukadirisho wa jamii mbali mbali yanayohusiana na utumishi na utoaji huduma. NRCEMH imefanya kazi muhimu, ikishirikiana na Kitengo cha Maelezo ya Takwimu {Information Statistics Division (ISD)}, katika utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Edinburgh kilitafuta njia za kupanga twakimu za afya za jamii mbali mbali nchini Scotland.

Website inatayarishwa kwa nia ya kutoa maelezo kwa njia ya kiutaalamu.

Usimamizi wa Magonjwa ya Kila siku: Katika utaratibu wa Mpango wa Magonjwa ya Kisukari nchini Scotland (Scottish Diabetes Framework) chini ya kifungu cha 85, National Resource Centre for Ethnic Minority Health iliombwa itoe Ripoti kuhusu Elimu ya Magonjwa ya Mlipuko kati ya jamii za tabaka za walio wachache nchini Scotland. Matokeo ya mwanzo yatatolewa katika Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano utakaofanyika mwishoni wa mwaka 2003.

Haemoglobinopathies: Kikundi cha usimamizi kinachoangalia uchambuzi wa mahitaji ya uchunguzi wa ugonjwa huu.

SEHEMU YA 2

Sehemu hii inaelezea maendeleo yaliyofanywa na NHSScotland katika utekelezaji wa Haki bila Upendeleo HDL 2002 (51) pamoja na Taratibu za Haki bila Upendeleo.

Kifungu cha I: Haki Bila Upendeleo

Mkutano wa Haki bila Upendeleo Stocktake uliofanywa 2000 kuchunguza hali ya mitizamo ya mila na utamaduni ya mashirika ya NHS. Masuala haya manne muhimu yalitambuliwa: Haki bila upendeleo; Uongozi; Maarifa ya Upangaji na Majukumu. Utoaji wa muongozo wa HDL (2002) 51, utaratibu wa utimizaji baada ya miaka mitatu ulitolewa na Kamati ya Scotland kwa ajili ya NHSScotland. Kuipa nguvu chama kwa njia ya uongozi bora; kuchambua maelezo ya takwimu za jamii ambazo ziko kwenye hatari na kuangalia mahitaji ya afya ili kuendeleza upangaji mzuri; kukuza utoaji huduma kwa njia ya kuthibitisha utoaji wa huduma unaofuatana na mila na desturi pamoja na matakwa ya kidini; kukuza haki bila upendeleo haswa wakati wa kuajiri na uteuzi; na kukuza ustawi wa jamii kwa njia za kusikiliza na kuwajumuisha watu ili wapate maangalizi.

Kifungu cha II: Majibu ya NHSScotland kuhusu Haki bila Upendeleo na Mitizamo ya Mila na Utamaduni

Ingawa ukamilishaji wa mambo utachukua muda mrefu, kuna ushahidi unaonyesha msimamo mzuri wa maendeleo unaohusiana na masuala ya haki bila upendeleo ya NHS nchini Scotland, na mambo yanaanza kutegema ukilinganisha na kipindi kile cha Stocktake. Mameneja Watendaji wa NHS waliweka sahihi ya makubuliano ya 'Changamoto ya Uongozi' yaliyotolewa na Kamati ya Haki bila Upendeleo ili kuonyesha moyo wao wa kutekeleza suala hili.

Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipango Itakayofanywa: Mwanzoni kulikuwa na wasiwasi na ugumu wa kuelewa umuhimu wa maendeleo ya Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipango Itakayofanywa na Haki bila Upendeleo. Masuala hayo yaligusia hofu ya kutotekeleza mambo, ukosefu wa kuelewa kiini cha ubaguzi serikalini na vitendo vya ubaguzi na uhaba wa kumulika suala la 'jamii tofauti' kwa sababu ya idadi ndogo ya watu. Hata hivyo, Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipango Itakayofanywa na masuala ya Haki bila Upendeleo yalitimizwa kwa wakati mzuri. Kuna ushahidi wa maendeleo ya Kamati nyingi za afya haswa kama kuna wafanyakazi watiifu au/na kama kuna Katibu Mkuu mwenye shauku kubwa ya kazi. NRCEMH ilitoa msaada na muongozo wa kuendeleza Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipango Itakayofanywa. Utaratibu wa Makadirio Nchini uliotayarishwa kwa ushirikiano na CRE unatumia kusaidia kutambua sehemu zinazohitaji maendeleo.

Uchunguzi uliofanywa nchini – muhtasari na malengo: Uchunguzi uliofanywa nchini kuhusu Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipango ulitekelezwa na NRCEMH wakishirikiana na CRE. Ripoti kamili itatoa muongozo utakaosaidia Kamati na Tume ili ziweze kutekeleza Taratibu za Haki bila Upendeleo na Mipangilio. Pia itasaidia kutoa mwelekeo wa baadaye wa shughuli za NRCEMH kwa kumulika maeneo na masuala muhimu ya maendeleo pamoja na muongozo wa sera utakaotekelezwa na NRCEMH. Maeneo hayo ni pamoja na: ushauri; ustawi wa jamii; utoaji huduma; utumishi; wakala; makadirio ya matokeo; vifaa vya ukaguzi wa takwimu na vielelezo vya utendaji.

Ushirikiano na NRCEMH: Ushirikiano kati ya NRCEMH na Kamati na Tume za Afya unaendelea vizuri na kuna juhudi kubwa za mashirika na vikundi vya watenda kazi. Maombi ya watu binafsi wanaohitaji ushauri na msaada yameongezeka.

Mashirika: Madhumuni na shughuli za wakilishi wa Shirika Tawala zinaendelea. Maendeleo hayo yalisaidiwa na matembezi yaliofanywa na wafanyakazi wa NRCEMH katika Kamati kadhaa za Afya. Mpango wa NRCEMH unatekelezwa kwa kutumia mtandao wa habari, mafunzo na maarifa pamoja na utendaji wa shughuli za ushirikiano zinazosimamiwa na Kamati pamoja na Tume.

Changamoto: Tatizo mojawapo ni namna ya kwenda sambamba na mabadiliko ya kisiasa haswa wakati wa kufuatilia Maelekezo ya EU pamoja na ushauri wa Kamati ya Haki bila upendeleo; umuhimu wa kuzingatia haki bila Upendeleo kwa ujumla ikiwa ni mojawapo ya wajibu wa jumua; kujishughulisha na ubaguzi uliopo serikali; kuendeleza mawasiliano kati ya mashirika na kuhakikisha kuna mabadiliko yanayopimwa.

Mwelekeo: NRCEMH utashawishi ujumuikaji wa jamii za tabaka za walio wachache ili kuhakikisha ya kwamba wanapewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ya NRCEMH. Itaendelea kutia mkazo suala la ushirikiano na kutafuta njia bora za utendaji na jinsi ya kutoa nafasi kwa wote. NRCEMH itashiriki kutoa muongozo nchini, kutoa vielelezo vya utendaji na malengo, kupima mabadiliko ya utendaji; na kufanya shughuli zinazohusiana na jamii tofauti nchini kama vile Kuzingatia Wagonjwa na Ushirikisho wa Umma.

Mashirika muhimu ya afya yanayosaidiwa na NRCEMH ni Kamati pamoja na Tume za NHS. Lakini, NRCEMH inajenga uhusiano bora na vyama vya kujitolea, serikali za mitaa na vyombo vingine vya serikali.

Mwisho

Moyo wa kufanya kazi, usimamizi mzuri, muongozo wa kudumu ya masuala fulani na muongozo wa sheria, na nia ya kutenda mema katika NHS, imeifanya Scotland iwe na maendeleo mazuri ya kukabili sera ngumu na migogoro inayoletwa na jitihada za kutimiza malengo ya kuunda huduma ya afya inayofuatana na mila na desturi za jamii tofauti, na za jumua tofauti. Ili msimamo huu uendelee, utaratibu lazima uonekane ni wa kudumu na unahitaji kutilia mkazo masuala muhimu yaliyokubaliwa kwa ushirikiano na watu mbali mbali.

Tumetimiza Maangalizi ya Mwaka ya Kamati ya mwanzo yanayohusiana na haki bila Upendeleo. Masuala muhimu ya uchunguzi huo yatatusaidia kuzingatia shughuli za mwaka wa 2 na wa 3:

- Tukishaweka uongozi bora katika ngazi za juu tutapenda kuona usimamizi mzuri wa wakurugenzi na wafanyakazi.
- Kamati zimechukua maelezo ya jumua na zimefanya makadirio ya mahitaji ya jamii za tabaka za walio wachache. Kwa hiyo tunahitaji vifaa mbali mbali vya kutusaidia kurekebisha utaratibu wa kuchambua mafanikio ya shughuli za afya pamoja na kuimarisha utaratibu wa kufanya utafiti.
- Action Plans imetambua kuna mapengo yanayotakiwa kuangaliwa; Kamati itapewa ushawishi wa kujiendeleza haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha ya kwamba huduma zinatolewa kufuatana na mila na desturi haswa kwa upande wa mawasiliano, chakula, matakwa ya kidini na ushauri.

- Utoaji wa mafunzo na ufundishaji utahitaji mpangilio mzuri katika kila hatua; mafunzo, wafanyakazi wenye uzoefu, maarifa ya kufuta ubaguzi yatakayotekelezwa na wakurugenzi, maendeleo ya kazi na uwezo wa kuwashauri wafanyakazi wa jamii za tabaka walio wachache.
- Msaada na muongozo utatolewa kufuatana na ushauri mzuri na ushirikiano na kufuatana na matakwa ya wahudumiwa wa jamii za tabaka za walio wachache; kutakuwa na uwezo wa kufanya ushirikiano kati ya maeneo tofauti na kuabatanisha njia tofauti za kutenda kazi.
- Tutahakikisha ya kwamba masuala ya haki bila upendeleo yataingizwa ndani ya mipango ya vijijini na mashirika mbali mbali, na pia mahitaji ya jamii za tabaka za walio wachache yataangaliwa ikiwa ni mojawapo ya majukumu ya jumua.

Lengo kubwa la NRCEMH linajulikana wazi. Mojawapo ya shughuli muhimu za mwaka unaokuja ni kuimarisha muundo msingi wa Kamati za Afya za NHS zinazoshirikiana. Lengo hili na vingenevyo vitataka ushirikiano wa Kamati ya Scotland, mashirika na vyama vya wafanyakazi, pamoja na vyama vya wafanyakazi ingawa – muhimu zaidi – wagonjwa. Hatuwezi kuridhika upesi kwa sababu kazi ngumu ni kukamilisha kila hatua, ndio kwanza tumeanza.